**Learning by Ear – Climate Change**

**Episode 06**

**Text: Victoria Averill**

**Editing: Johannes Beck**

**Kisuaheli:Eric Ponda**

CHARACTERS:

Scene 1:

- LORNA (16)
- CAROL (14)
- NEWSREADER (FEMALE, ADULT)
- JOSHUA (15)
- ALEX (15)

Scene 2:

- CAROL (14)
- FARMER (MALE, ADULT)
- JOSHUA (15)

Scene 3:

- LORNA (16)

- HOTEL MANAGER (MALE, ADULT)
- ALEX (15)

Scene 4:

- LORNA (16)
- CAROL (14)
- ALEX (15)
- JOSHUA (15)

**Intro:**

Hujambo msikilizaji wa Deutsche Welle na karibu kwa makala ya sita ya mchezo wa "Radio Noa Bongo Jenga Maisha yako" bado tukiwa tunazungumzia mabadiliko ya hali ya hewa.Hatimaye Lorna anachukua uamuzi mgumu huku jopo kazi la wanafunzi wenzake likivumbua mengi kuhusu kawi inayoweza kutumika tena na tena na isiyochafua mazingira. Kwa mengi zaidi endelea kuwa nasi hadi mwisho wa kipindi.

## Scene One: Lorna’s House

| | |
|---|---|
| **SFX ATMO:** | **TV IN BACKGROUND** |
| **1. LORNA:** | Sasa tufanyeje? Siamini kwamba sisi ni walengwa kutokana na msimamo wetu na juhudi za kukabiliana na mabdiliko ya hali ya hewa na ongezeko la kiwango cha joto ulimwenguni- Ni vile…….. … |
| **SFX** | **NEWS BULLETIN** |
| **2. NEWSREADER:** | Wakulima barani Afrika wamekuwa walengwa kama washirika wakuu katika juhudi za kupambana na mabadiliko ya hali ya hewa.. |
| **3. CAROL:** | Hebu ngoja kidogo Lorna, tusikilize hii taarifa. |

**4. NEWSREADER:** Juhudi za kutafuta nishati mbadala inayoweza kutumika tena na tena barani Afrika sasa inawalenga wakulima kama watoaji wa nishati inayotokana na mimea. Nishati hii huzalishwa kutokana na mazao kama vile ngano, miwa na mmea aina ya ***Jatropha*** …

**SFX:** **NEWSREADER VOICE AS BED UNDER**

**5. JOSHUA:** Nishati ya mimea? Hiyo ndiyo mtaalam wa mazingira aliyokuwa akizungumzia.

**6. LORNA:** Joshua, unadhani nishati inayotokana na mimea inaweza kuwa njia mbadala kutumiwa katika viwanda vya kuzalisha umeme?

**7. ALEX:** Nani ajuaye Lorna?

| | |
|---|---|
| **8. LORNA:** | Sawa Alex. Sasa nimekata kauli! Tutaendelea na vita dhidi ya ujenzi wa kiwanda hiki. Sharti wahusika wazingatie usafi wa mazingira au tusimamishe kabisa mradi huu. Tumekubaliana? |
| **9. JOSHUA/CAROL:** | Ndio! |
| **10. ALEX:** | Sawa basi. Lakini Carol ni lazima tuwe waangalifu! |
| **11. CAROL:** | Napendekeza tufanye utafiti haraka iwezekanavyo kuhusu nishati ya mimea ili tupate habari kamili kabla ya kuendelea na maandalizi ya maandamano yetu. Tuko na siku tatu pekee zilizosalia. |

## Scene Two: Jatropha Nursery

**12. CAROL:** Kwa hivyo hii misitari yote ni mmea wa ***Jatropha***?

1**3. FARMER:** Ndio. Nilianza kuipanda miaka michache iliyopita kwa ufadhili wa benki ya dunia. Nilisikia kuhusu mradi huu redioni kuhusu umuhimu wa kutafuta njia mbadala ya nishati mbali na mafuta ya petroli, na kwamba aina hii ya nishati inaweza kuwa suluhisho!

**14. JOSHUA:** Lakini nishati ya mimea ni nini hasa?

**17. FARMER:** "Nishati ya mimea huzalishwa kutokana na mchanganyiko wa aina mbalimbali ya nishati - mafuta ya mboga na matunda, wanyama, spiriti, dizeli kutoka kwa mimea" Malighafi hii kisha husagwa ili kutoa mafuta mengi inavyowezekana.

**18. CAROL:** Kwa hivyo mafuta haya yanayoweza kutumiwa kuendesha gari dogo au basi hutoka viwandani?

**19. FAMER:** Ndio. Mara nyingi, mafuta haya hutumiwa moja kwa moja na wenye magari iwapo injini ya gari imefanyiwa marekebisho ili kuweza kutumia mafuta haya. La sivyo unapasa kuyachuja zaidi au kuyachanganya na mafuta ya petroli ya kawaida.

**20. CAROL:** Kwa hivyo mafuta haya hutokana na mimea. Lakini manufaa yake ni nini?

**21. FARMER:** Mafuta haya yanaweza kutumiwa tena na tena. Yaani unaweza kupanda mimea na kuivuna mara kwa mara kinyume kabisa na makaa ya mawe ambayo yanatumiwa mara moja tu. Na mafuta haya hayatoi moshi au gesi inayochafua mazingira ikilinganishwa na mafuta ya diesel au petroli.

**22. JOSHUA:** Na kwa nini unapanda mumea huu wa ***Jatropha?***

**23. FARMER:** Mmea huu hukua kwa haraka na huchukua muda mfupi kukomaa. Mbali na hayo unaweza kustahamili ukame kama inavyoshuhudiwa katika sehemu nyingi barani Afrika. Wataalam wanaamini kuwa mmea huu unaweza kuzuia kuenea kwa jangwa.

**26. JOSHUA:** Swali lingine! Kwa mfano, iwapo wakulima kama wewe watatayarisha mashamba yao kwa ajili ya kupanda… tuseme mahindi, mawele, ngano na nafaka nyinge, kisha wabadili na kuanza kukuza ***Jatropha,*** nani atakayelisha taifa?

**27. FARMER:** Nilipoanza kukuza mmea huu wa ***Jatropha,*** haikuwa kazi rahisi lilikuwa tatizo. Lakini, kwa wakati huu wakulima wengi wameingilia kilimo hiki na huenda ikasababisha matatizo.

**28. CAROL:** Ndio. Katika siku za hivi punde tayari bei za vyakula zimepanda na endapo wakulima wataanza kuzingatia zaidi kilimo cha kukuza mimea kuzalisha kawi, bei za vyakula zitaendelea kupanda.

**29. FARMER:** Mmm, pengine. Lakini sasa pato langu limeongezeka kutokana na kilimo hiki cha ***Jatropha.*** Nimeweza kulipa karo ya watoto wangu, kuliko zamani nilipokuwa nikipanda mahindi. Sawa, sasa nitakuacha nirudi kazini. Kwaherini!

**30. JOSHUA:** Kwaheri.

**31. CAROL:** Sasa nimechanganyikiwa hata zaidi. Nishati ya mimea yaonekana ni wazo zuri na njia bora ya kukabiliana na mabadiliko ya hali ya hewa. Likini njia hii ya uzalishaji umeme inaonekana bado ina athari zake.

**32. JOSHUA:** Carol, naelewa. Lakini lazima tutafute njia nyingine zaidi kukabiliana na athari hizi …

## Scene Three: Outside Eco Hotel Palm Bay

**SFX ATMO** **HOTEL RECEPTION**

**33. LORNA:** Sasa unaona bosi! Maandamano haya huenda yatapita nje ya lile lango la hoteli, lakini nakuhakikishia hakuna shida itakayotokea. Tunataka kuhakikisha kuwa wafanyabiashara wote hapa wamefahamishwa kuhusu suala hili.

| | |
|---|---|
| **34. HOTEL MANAGER:** | Mimi siwezi kushiriki maandamano haya, lakini namhakikishia mke wangu ataungana nanyi. Mimi napinga kabisa ujenzi wa kiwanda hiki cha umeme. Ni makosa makubwa! Na unajua, si vigumu kupata nishati inayoweza kutumika tena na tena. Sisi hapa hotelini tayari tumeweka mtambo huo. |
| **35. LORNA:** | Kweli? Ulifanya vipi? |
| **36. HOTEL MANAGER:** | Hebu njoo hapa nje! |
| **SFX** | **Walking outside** |
| **SFX ATMO** | **GARDEN/BIRDS** |
| **37. HOTEL MANAGER:** | Unaona zile paneli nyeusi kwenye paa? Zinatumika kuzalisha nishati ya jua. Hapa tumebarikiwa na mwanga wa jua kwa mwaka mzima, kwa hivyo nishati tunayotumia sana hotelini inatokana na miale ya jua. Kupitia mnunururisho huibadilisha miale ya jua na kuwa nishati … |

**38. ALEX:** Kufanya nini?

**39. HOTEL MANAGER:** Tuna paneli zinazotumiwa kuchemsha maji, nyingine kuzalisha umeme unaotumika kwa taa zetu na pia hutumia glopu zisizotumia kiwango kikubwa cha umeme.

**40. ALEX:** Na je wakati kunaponyesha? Kwa mfano wakati wa msimu wa mvua ambapo kunakuwa mawingu kwa wiki nzima?

**41. HOTEL MANAGER:** Nishati ya jua, huwa haitegemei miale ya moja kwa moja – ili mradi tu kuna mwangaza, nishati hiyo itazalishwa.

**42. LORNA:** Nafurahi sana kusikia jambo hilo. Lakini nishati hii ya jua inaweza kutoa umeme wa kutosha katika kiwanda hiki cha Dhowville?

**43. HOTEL MANAGER:** Nadhani inaweza. Nimesoma kuhusu viwanda vikubwa vinavyozalisha nishati ya jua, vikifanyiwa majaribio nchini Uhispania. – huvuta miale ya jua kwa kutumia vioo vikubwa na kutumiwa kuchemsha maji kuyageuza kuwa gesi ya moto inayotumiwa kuendesha matabo viwandani. Kwa hivyo, unaweza kuzalisha umeme wa kutosha kwa mji mdogo.

**44. ALEX:** Basi yaonekana ni gharama kubwa kujenga na kuweka vifaa hivi!

| | |
|---|---|
| **45. HOTEL MANAGER:** | Nishati ya jua bado ni ghali, hilo ni kweli! Maana gharama yake ni maradufu ya ile inayotokana na makaa ya mawe au gesi. Ni suluhisho zuri kwa vijiji vidogo ambavyo havijaunganishwa na huduma za taifa. Lakini kwa viwanda vikubwa gharama ni kubwa mno. Pia kuna nishati nafuu kama vile nishati ya upepo, maji na mvuke kutoka ardhini inayoweza kutoa kiwango kikubwa cha umeme. |
| **46. LORNA:** | Wow, kwa hivyo kuna njia njingi tu za kuzalisha nishati! Nadhani tunahitaji kufanya utafiti zaidi kuhusu suala hili. Asante kwa habari hizo. |
| **47. HOTEL MANAGER:** | Nawatakia kila la kheri katika maandamano yenu na muendelee na kazi hiyo nzuri. |

**Scene Four: Lorna’s House**

**SFX ATMO:** **RADIO/MUSIC**

**48. LORNA:** Ok, sasa tunahitaji kutayarisha mabango haya yaonekane ya kitaalam kabisa. Carol, unaweza kusoma maandishi.

**49. CAROL:** Sawa, ninayawagawanya kwenye kaulimbiu tatu. ***“Kiwanda kinachojali mazingira la sivyo hakuna kiwanda cha umeme”. “Komesha mabadiliko ya hali ya hewa.” “Kataa kiwanda cha umeme”. “Komesha mabadiliko ya hali ya hewa - Kiwanda kinachojali mazingira la sivyo kiwanda kisijengwe.”***

**50. LORNA:** Vyema kabisa!

| | |
|---|---|
| **51. JOSHUA:** | Pia yanahitaji kuchapishwa kwa maandishi makubwa kama lile bango alililotengeneza Alex. Kisha waandishi wa habari watakapofika wanaweza kuyapiga picha kwa urahisi. |
| **52. LORNA:** | Lakini Carol, uliwasilisha barua ya kuwaalika waandishi wa habari? |
| **53. CAROL:** | Lorna, kila kitu kimekamilika. Na bado naendela kusambaza vipeperushi katika vibanda ya kuuzia magazeti. Bila shaka watu wengi watajitokeza kutuunga mkono. |
| **SFX** | **CLUNK SOUND AS POWER CUT** |
| **54. LORNA:** | Lakini hilo linachukiza sana. Umeme umekatika! Nitawasha jenereta tu! |
| **55. JOSHUA:** | Lorna, Siamini una jenereta! |

**56. LORNA:** Kwa nini Joshua? Mamangu anaweza kugharamia mafuta!

**57. JOSHUA:** Sio kuhusu gharama, lakini mafuta ya jenereta hutoa moshi na gesi chafu inayochafua mazingira na kuongeza kiwango cha joto duniani.

**58. CAROL:** Ni kweli!

**59. LORNA:** Sasa tutafanyaje – Tukae gizani?

**60. JOSHUA:** Itabidi.

**61. LORNA:** Mmm, Nadhani mimi na mama tunapaswa kutenda yale tunayohubiri. Unahakika hutaki tuwashe jenereta, angalau tumalize kazi yetu ya kutayarisha haya mabango?

**62. ALEX:** Ok, Sawa basi tutakuruhusu kwa mara hii moja tu!

**63. LORNA:** Alex, haitachukua muda mrefu, sawa?

| | |
|---|---|
| **SFX** | **DOOR SLAMMING** |
| **64. LORNA:** | **(scream)** Nisaidieni! Haraka nisaideini tafadhali! **(shouting from outside)** |

**END OF EPISODE 6**

**Outro:**

Na hadi hapo tumefika mwisho wa kipindi hiki cha Noa Bongo Jenga Maisha yako kwa leo. Ungana nasi wakati mwengine ufahamu yatakayompata Lorna, na iwapo jopo kazi la wanafunzi litaendelea na mipango ya kuandaa maandamano yao

Mchezo huu kuhusu mabadiliko ya hali ya hewa umeandikwa na Victoria Averill. Na kumbuka ukipenda kusikiliza tena kipindi hiki, usikose kutembelea tovuti yetu: www.dw-world.de/lbe Hadi wakati huo basi kwaheri kwa sasa.!